JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

# SHERIA BULLETIN

Toleo la Kumi




MAMA SAMIA Legal Aid Campaign

## YALIYOMO


01 | Tushirikiane Kutekeleza MSLAC Singida

04 | MSLAC Yaamua Mgogoro wa Familia

08 | Wananchi Washauriwa Kuibua Kero Nzito Nzito Kuitwisha MSLAC



## BODI YA UHARIRI

**MARY MAKONDO**
Katibu Mkuu

**LUSAJO MWAKABUKU**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAJUMBE**
William Mabusi | Ibrahim Joseph

**WASANIFU WA KURASA:** Waziri Bosco

# **Tushirikiane Kutekeleza MSLAC Singida:** Dkt. Kazungu



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Dkt. Khatibu Kazungu akizungumza na Sekretarieti ya Mkoa wa Singida kufanya tathmini ya maandalizi ya MSLAC mkoani humo, 04 Januari, 2024, Singida.

**Na William Mabusi**
- WKS Singida

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Dkt. Khatibu Kazungu ametoa wito kwa Mkoa wa Singida kutoa ushirikiano wa kutosha wakati wote wa utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Campaign - MSLAC) inayotegemewa kufanyika mkoani humo kuanzia tarehe 10 hadi 19 Januari, 2024.

Dkt. Kazungu ametoa wito huo alipokutana na kufanya mazungumzo na Sekretarieti ya Mkoa wa Singida tarehe 04 Januari, 2024 kwenye ofisi za Mkuu wa Mkoa, akiwa ameongozana na sehemu ya Menejimenti ya Wizara. Kikao kazi hicho kililenga kufanya tathmini ya awali ya maandalizi ya MSLAC ambayo itatekelezwa kwenye Halmashauri zote saba mkoani humo.

"Kikubwa ambacho Wizara inaomba kutoka kwenu ni ushirikiano mkubwa ili kufanikisha Kampeni hii. Kote ambako tumetekeleza kampeni hii tumepata ushirikiano wa kutosha na sasa ni zamu yenu." Alisema na kuongeza kuwa wananchi wahamasishwe kufika kwa wingi siku ya uzinduzi lakini pia kwenye maeneo ambayo mikutano ya kutoa elimu na huduma ya msaada wa kisheria itakuwa inafanyika.

Akitoa maelezo ya maandalizi yaliyofanyika kwa upande wa mkoa, Msajili Msaidizi wa Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria mkoani humo Bi. Shukrani Mbago amesema Halmashauri zote saba zimetaarifiwa kuhusu kufanyika kwa kampeni hiyo, Kata zote ambazo zitapitiwa na kampeni zimeshaandaliwa, wamekaa na Watoa huduma za kisheria, mkoa umeunda Kamati ya maandalizi ya uzinduzi wa Kampeni. Aidha, mialiko mbalimbali imetolewa kwa Taasisi na Wadau muhimu wanaotakiwa kushiriki Kampeni pamoja na maandalizi ya bajeti ya kutekeleza Kampeni mkoani humo.

Akiongea kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Bw. Stanslaus Beatus Choaji amesema Mkoa wake utafanya yote yanayohitajika kufanya kampeni hiyo itekelezwe kama ilivyopangwa. Aidha, ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuja na mpango huu wa kutetea haki kwa wananchi wanyonge.



Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Bw. Stanslaus Beatus Choaji akitoa neno la ukaribisho kwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Dkt. Khatibu Kazungu ili aongee na Sekretarieti ya Mkoa, 04 Januari, 2024, Singida.



Wajumbe walioshiriki kikao cha tathmini ya maandalizi ya MSLAC mkoani Singida wakimsikiliza Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Dkt. Khatibu Kazungu, 04 Januari, 2024, Singida.

# Serikali itaendelea kulinda na kukuza upatikanaji haki – Dkt. Chana



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akiwasili viwanja vya Stendi Mpya ulipofanyika uzinduzi wa Utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, 10/01/2024 Mkoani Singida.



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akiashiria "kazi nzuri" alipotembelea banda la Wizara ya Katiba na Sheria kabla ya uzinduzi wa Utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, 10/01/2024 Mkoani Singida.

**Na William Mabusi**
– WKS Singida

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana amesema Serikali itaendelea kulinda na kukuza upatikanaji haki nchini kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ya kisera ya Kitaifa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kunakuwa na usawa mbele ya sheria, wananchi wanalindwa na wanapata haki kupitia vyombo vya haki.

Dkt. Chana ameyasema hayo Mkoani Singida alipokuwa anazindua utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ijulikanayo kama Mama Samia Legal Aid Campaign iliyoanza kutekelezwa mkoani humo leo tarehe 10 Januari, 2024.

"Lengo la utekelezaji wa kampeni hii ni kulinda na kukuza upatikanaji wa haki kwa wote kupitia huduma ya msaada wa kisheria nchini ambayo ni utekelezaji wa Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ibara ya 8 (1) (b) na Ibara ya 13 (1) zinazoweka msingi wa haki na usawa na ustawi wa wananchi. "

Ameyataja mafaniko makubwa yaliyopatikana tangu kuanza kutekelezwa kwa kampeni hiyo mwezi Aprili 2023 hadi kufikia Oktoba, 2023 ambapo jumla ya mikoa mitano imeshatembelewa, kuwa ni pamoja na jumla ya migogoro 6,365 iliyohusu masuala ya ardhi, ndoa, mirathi na matunzo ya watoto ilipokelewa ambapo kati ya hiyo migogoro 488 ilitatuliwa na kuhitimishwa. Migogoro 5,877 inaendelea kushughulikiwa katika mamlaka mbalimbali za kimahakama na kiutawala na Wizara kupitia Waratibu na Wasajili wa mikoa na wilaya imeendelea kufuatilia utekelezaji wake.

Aidha, wananchi 2,055 (Wanaume1,035 Wanawake 1,020) walisajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa kupitia Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu – RITA, kumekuwepo na ongezeko la uelewa na uwajibikaji wa Watendaji wa Vijiji, Kata, Halmashauri, Viongozi wa kidini na kimila, Wanafunzi na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari katika kuwahudumia wananchi na kuwasaidia kudai na kupata haki zao baada ya kujengewa uwezo katika masuala mbalimbali ya sheria, haki za binadamu na utawala bora.



Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania Prof. Elisante Ole Gabriel akifafanua jambo kwa Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana kwenye Banda la Mahakama kabla ya uzinduzi wa Utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, 10/01/2024 Mkoani Singida.

Kampeni ya Msaada wa Kisheria inatokana na adhma ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha kwamba kila mwananchi anafahamu masuala ya kisheria ikiwemo haki na wajibu wake na kwamba kila mwananchi anaifikia haki na wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za Mawakili waweze kufikia haki kupitia huduma za msaada wa kisheria.

Kupitia kampeni hiyo, msaada wa kisheria unatolewa bure katika Halmashauri zote saba za Mkoa wa Singida hadi tarehe 19 Januari, 2024, lengo likiwa ni kufikia jumla ya Kata 70 na vijiji 210. Hivyo wananchi wote wa Mkoa wa Singida kwenye kata ambazo kampeni hiyo itafanyika wameombwa kuitumia fursa hiyo kwa kuhakikisha kuwa wanashiriki kikamilifu kwa kupata elimu na huduma mbalimbali za masuala ya kisheria zitakazotolewa. Aidha, amewasihi viongozi wa maeneo hayo kutoa ushirikiano wa kutosha kwa wataalam wanaotekeleza kampeni.

Akimkaribisha Mgeni Rasmi, Mkuu wa Mkoa wa Singida Bw. Peter Serukamba amesema mkoa ulianza maandalizi ya kuipokea kampeni tangu ilipozinduliwa mwezi Aprili 2023 Jijini Dodoma. Ameongeza kuwa kila Halmashauri ina watoa huduma ambao wamepata mafunzo ya kutekeleza kampeni hiyo hivyo wataitumia fursa hiyo ipasavyo kwa mustakabali wa kuendeleza amani ya mkoa na kumaliza migogoro inayochelewesha shughuli za maendeleo.



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akiteta jambo na Mkuu wa Mkoa wa Singida Bw. Peter Serukamba kwenye mkutano wa uzinduzi wa Utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, 10/01/2024 Mkoani Singida.



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akihutubia wakati anazindua utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, 10/01/2024 Mkoani Singida



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana na Meza Kuu kwenye picha ya pamoja na watumishi wa Wizara ya Katiba na Sheria, 10/01/2024 Singida.

# MIGOGORO YA ARDHI KERO SUGU IRAMBA



Mkuu wa Wilaya ya Iramba ,Suleiman akizungumza na wananchi wa Kata ya Shelui Wilaya ya Iramba Mkoani Singida kwenye mkutano Kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia uliofanyika Kijiji cha Nselembwe Wilayani humo tarehe 11/01/2024

**Na Ibrahim Joseph**
- SINGIDA.

MIGOGORO ya ardhi imetajwa kuwa ni ndio moja ya kero kubwa kwa wananchi wilayani Iramba Mkoani hapa na imesababisha kutumia muda mwingi kutafuta haki hiyo maeneo mbalimbali ya utoaji haki.

Hayo yalibainishwa wakati wa mkutano wa hadhara kati ya wananchi na timu ya kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia uliofanyika Kata ya Shelui Wilaya ya Irimba Mkoani Singida.

Kero hiyo ya migogoro ya ardhi imetajwa kuwa ni kubwa kwa wananchi hao na imesaababisha kutumia muda mwingi kuitafuta haki hiyo kwenye maeneo ya utoaji haki. Mmoja wa wananchi wa Kata hiyo Johashi Shimikila akizungumza kwenye mkutano huo alisema kero hiyo inaongoza kati ya kero nyingi walizonazo wananchi wa wilaya hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Iramba ,Suleiman akizungumza na wananchi wa Kata ya Shelui Wilaya ya Iramba Mkoani Singida kwenye mkutano Kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia uliofanyika Kijiji cha Nselembwe Wilayani humo tarehe 11/01/2024

Shimikila alisema wanashuru wajumbe wa kampeni hiyo kufika hapo na kilio chao namba moja ni kero ya ardhi ambayo imesabaisha kupoteza mud na fedha kiitafuta. Kadhalika alisema wanamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kujna na kampeni hiyo ambayo inatoa fursa kwa wananchi kusikilizwa na kusaidiwa kupata haki zao

"Binafsi nimetoa kero yangu hii ambayo imekuwa ikinisumbua mimi na wananchi wenzangu ya migogoro ya ardhi hivyo kupitia kampeni hii nimepata Imani ya kuhudumiwa "alisema.

Aliitaja aina ya migogori iliyopo kuwa ni kugombea mipaka ya mashamba na wengine kudhulimiwa ardhi kutokana na kushindwa kuwalipa mawakili wa kuwasaqidia kesi zao.

Aliongeza migogoro mingine ni kucheleweshwa kwa hati za maeneo yao waliopimiwa jambo ambalo linawachelewesha kuendeleza maeneo yao . Mkazi mwingine Sada Salula alisema wanawake wengi waliofiwa na waume wao hasa maeneo ya Vijijini wamekuwa wakinyang'anywa ardhi kwa madai kuwa hawana haki ya kumiliki.

Sada alisema wajane hao wamekuwa wakifukuzwa kwenye familia waliyokuwa wakiishai na wenzao wa kwa madai kuwa mila haziruhusu mjane kumiliki ardhi.

"Mimi hapa ni miongoni mwa wajane niliyenyang'anywa ardhi baada ya mume wangu kufa kwa sa nahangaika na watoto wangu nimeshafukuzwa nimeona nifike hapa kutoa kilio change kwenye kampeni hii ya Mama Samia"aliangua kilio.
Mkuu wa Wilaya ya Iramba ,Suleiman Mwenda alikiri kuwepo kwa malalamiko hayo ya ardhi na kuwataka wananchi kufika kwenye kampeni hiyo ili kupata haki yao.

"Kwa kweli katika malalamiko mengi yanayokuja ofisini kwangu kama Mkuu wa Wilaya ni masuala ya ardhi,ardhi imekuwa tatizo sana katika wilaya yetu ya Iramba ,kesi ni nyingi mno kutokana na uhaba wa watoa huduma za kisheria kumeibuka na wanasheria feki wanaowatapeli wananchi"alisema

Mwenda alisema anaamini kupitia kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria mama Samia itawasaidia wananchi wengi kupata haki zao kwa sababu inawataalamu wa kila idara na aliwataka wananchi ahao kujitokeza mbele ya timu hiyo ili kusikiliza na kutatuliwa kero zao zinazowakabili.

Kiongozi wa kampeni ya huduma ya msaadw wa kisheria ya mama Samia Wilaya ya Iramba ,Godfrey Ngangaji alisema kampeni hiyo ilizinduliwa Aprili 2023 na inaendelea kuzinduliwa kila Mkoa mpaka sasa imefika Mikoa sita.

Ngangaji alisema lengo la kampeni hiyo ni kuwasaidia wananchi kupata haki zao na imekuwa ikifanyakazi na watu wa idara zinazotoa haki ambazo ni mahakama,wanasheria,jeshila Polisi,Maofisa maendeleo ya jamii,Ustawi wa jamii ,Ofisi ya Mwendesha mashtaka na watalamu wengine wa sheria.



Baadhi ya wananchi wa Kata ya Shelui Wilaya ya Iramba Mkoani Singida wakiwasikiliza wataalamu wa msaada wa kisheria kutoka Kampeni ya Mama Samia uliofanyika jana Wilayani humo.

# MSLAC Yaamua Mgogoro wa Familia Uliodumu Miaka Mitatu



Timu ya MSLAC inayotekeleza kampeni hiyo katika Halmashauri ya Ikungi ikiwa katika kikao kutatua mgogoro kati ya Bw. Temistocules Kokula na mkewe Bi. Neema Joseph, tarehe 13 Januari, 2024

**Na William Mabusi**
- WKS Singida

Kampeni ya Kitaifa ya msaada wa kisheria ya Mama Samia Legal Aid Campaign (MSLAC) inayoendelea kutekelezwa mkoani Singida imeamua ugomvi na kuunganisha familia ya watoto saba ya Bw. Temistocules Kokula na Bi. Neema Joseph wa kijiji cha Mwisi Kata ya Lighwa Halmashauri ya Ikungi. Ugovi wa muda mrefu uliokuwa unapelekea vipigo kwa Bi. Neema na watoto ulimfanya aondoke kurudi kwao mwaka 2021 na kuwaacha watoto ambao wamekuwa wakimtoroka baba yao na kumfuata kutokana na malezi ya baba ambayo yamekuwa ya vipigo vya mara kwa mara.

Mgogoro huo uliibuka baada ya Bw. Kokula kufika kwenye timu ya MSLAC akilalamika kuwa watoto wake wamemtoroka na kurudi kwa mama yao. Ili kujua undani wa mgogoro huo, timu ya MSLAC chini ya Mratibu wake Wilayani humo Bw. Laurent Burilo iliwaita wanandoa hao kwenye kikao.

Haikuwa kazi rahisi kumshauri Bi. Neema kurudi kwa mumewe ili kuwalea watoto, hata hivyo baada ya wote wawili kupewa elimu sheria na madhara ya ukatili wa kijinsia na timu ya MSLAC ambayo pamoja na wataalam wengine lakini pia inaambatana na Afisa Ustawi wa Jamii, Afisa Polisi kutoka Dawati la Jinsia na Watoto walielewa na Bw. Kokula kukiri kuwa wataenda kuishi kwa amani.

Akihitimisha mgogoro huo Afisa wa Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto Bi. Dalahile Mahende kutoka Halmashauri ya Ikungi amesema Ofisi yake kwa kushirikiana na Ofisi ya Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Ikungi wataendelea kufuatilia mwenendo wa familia hiyo na endapo ikibainika kuendelea kwa vitendo hivyo, hatua zaidi za kisheria zitachukuliwa.



Timu ya MSLAC inayotekeleza kampeni hiyo katika Halmashauri ya Ikungi ikishangilia baada ya kumaliza mgogoro kati ya Bw. Temistocules Kokula na mkewe Bi. Neema Joseph, tarehe 13 Januari, 2024

# WATOTO WAJITUNZA WENYEWE MIAKA MITATU



Timu ya Kampeni ya huduma ya masada wa kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Campain) wakishangilia baada ya kufanikiwa kuwaunganisha tena Temistocules Ijengo na Neema Joseph (walioshikana mikono) ambao walitengana katika ndoa yao kwa muda wa miaka mitatu na kusababisha watoto wao saba wakiishi kwa kujitunza wenyewe kwa muda huo.

**NA Lusajo Mwakabuku & Ibrahim Joseph**
– Singida.

FAMILIA ya watoto saba wenye umri chini ya miaka 10 wamekuwa wakijitunza wenyewe kwa muda wa miaka mitatu kutokana na wazazi wao wakutengana .

Watoto hao wameibuliwa na kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia inayoendelea wilayani hapa hapa baada ya kuzinduliwa januari 10 mwaka huu.
Timu ya wanahabari wa Mama Samia Legal Aid Campaign iilifanikiwa kuongea na mmoja wa watoto hao walipofika makao makuu ya wilaya ya Ikungi kukutana na timu ya kampeni hiyo iliyowaita baba mama na watoto hao wote ili kupata chanzo ya tattoo hilo .

Akizungumza tukio hilo mmoa wa watoto wa familia hiyo (jina linahifadhiwa) alisema wamekuwa wakijitunza kwa muda wote huo kutokana na wazazi wao kutengana na mama yao alikwenda kuishi nyumbani kwao.

Alibainisha kuwa wanakaa na baba yao anayeitwa Temistocules Ijengo na amekuwa hawahudumiaa kutokana na kushinda muda mwingi kwenye pombe hivyo hajui watoto hao kuwa wamekula nini .

Alisema mama yake aliondoka na kuwaacha watoto hao sita huku akimwacha mmoja wa watoto hao akiwa mdogo mwenye umri wa chini ya miaka miwili na alimtunza mpaka sasa ana umri wa miaka minne.

Aliongeza kwa sasa anasoma shule ya msingi lakini amekuwa haudhurii masomo vizuri kutokana na kutumia muda mwingi kuwahudumia wenzake kwa kuomba omba chakula kwa watu ili kuwatunza wenzake.

Pia alisema wakizidiwa na hali ya njaa wamekuwa wakienda kwa mama yao kuomba msaada wa chakula ili kujitunza na wamekuwa na tabia ya kumbakishia baba yao chakula kikipatikana kwa kuwa wanampenda na wasingependa kuona anakufa kwa njaa.

Kiongozi wa timu ya kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria Wilaya ya Ikungi, Laurent Burilo akizungumza na waandishi wa habari wilayani humo jana alisema kuwa wakiwa katika Kijiji cha Mwis



Kiongozi wa Kampeni ya huduma ya masada wa kisheria ya Mama Samia ,Malongo Jackson akitoa elimi ya msaada wa kisheria kwa wananchi wa Kijiji cha Ipande Halmashauri ya Wilaya ya Itigi Mkoani Singida walipofika mwisho wa wiki.

wilayani hapo kwa ajli ya kutoa elimu ya msada wa kisheria walipata taarifa ya watoto kupitia viongozi wa Kijiji hicho.

Burilo alisema baada ya taarifa hizo walichukua jukumu la kuanza kuwatafuta wazazi hao na walifanikiwa mwisho wa wiki kukutana nao na kufanya mazungumzo kwa wote wawili yaani Mke na mume.

Kadhalika alisema kuwa walianza kwanza kufanya mazungumzo na mmoja mmoja na kuwaeleza madhara ya maisha ya watoto wao na ndipo walipowakutanisha wote na kufanikiwa kuwaunganisha tena familia hiyo pamoja na watoto wao ambao nao walifika katika neo hilo.

Mmoja wa majirani wa familia hiyo Emanuel Ntandu ambaye naye alishiriki kuwasafirisha watoto hao pamoja na baba yao kutuka Kijijini kuwafikisha eneo hilo la makao makuu wa wilaya alisema wamekuwa wakiwasaidia chakula watoto hao mara kwa mara na wamekuwa wakilalamikia tatizo hilo kwa muda .

Aliishukuru kampeni hiyo ya mama Samia kwa kufika hapo na kuwasaidia watoto hao na ambao wameishi kwa shida wa muda huo wa miaka mitatu .

Mama wa watoto hao Neema Joseph akizungumza na waandishi wa habari alisema aliikimbia ndoa yake kutokana na unyanyasaji kutoka kwa mume wake Temistocules Ijengo .

Neema alisema siku ya mwisho kuondoka kwake hapo alishuhudia mume wake akiwapiga watoto na alipohoji naye alipigwa sana akaona bora aokoe uhai wake

Afisa Ustawi Wilaya ya Ikungi ,Beatrice Maeda alisema baada ya kufanikiwa kuwaunganisha tena familia hiyo wataendelea kuifuatilia na Temistocules atakuwa akiripotia ofisi ya Mtendaji wa Kijiji kila siku kwa muda wa mwezi moja kuangalia mwenendo wake na taarifa hizi zitakuwa zikifikishwa kituo cha polisi kila siku

Maeda endapo akikiuka masharti hayo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa sababu ndiye aliyeonekana kusababisha familia hiyo kutengana .

# ANDIKENI WOSIA KUEPUSHA MIGOGORO



Kiongozi wa timu ya Kampeni ya huduma ya masada wa kisheria ya Mama Samia kwa halmashauri ya wilaya ya Itigi, Malongo Jackson akitoa elimu kwa wananchi wa Kijiji cha Ipande halmashauri hiyo walipofika hapo kupitia Kampeni hiyo inayoendelea Mkoani Singida mwisho wa wiki

**NA Lusajo Mwakabuku**
**& Ibrahim Joseph**
– Singida.

JAMII imetakiwa kuandika wosia wa mali zao ili kuepusha migogoro ya mgawanyo wa mali hizo baada ya kifo cha mhusika kutokea. Ofisa kutoka Ofisi ya Wakala wa usajili ufilisi na udhamini (RITA) ,Mohamed Changula alitoa ushauri huo kwenye mkutano wa hadahara Kijiji cha Ipande halmashauri ya wilaya ya Itigi Mkoani hapa mwisho wa wiki walipofika kutoa elimu ya msaada wa kisheria kupitia kampeni ya mama Samia.

Changula alisema jamii inatakiwa kuandika wosia ili kupunguza migogoro ya mgawanyo wa mali baada ya kifo kutokea.

“Kuandika wosia sio kujichuria kifo kama jamii inavyoamini bali ni ustarabu wa kuandaa mgawanyo wa mali zako ili kuondoa mgogoro pale kifo kitakapokuchukua”alisema.



Kiongozi wa Kampeni ya huduma ya masada wa kisheria ya Mama Samia Wilaya ya Mkalama, Anthony Mbelwa akitoa elimu kwa wananchi wa Kijiji cha Mpambala wilaya hiyo walipofika hapo kusikiliza Kampeni hiyo inayoendelea Mkoani Singida juzi

Alitaja aina mbili za kuandika wosia kuwa ni kwa njia ya maandishi au na mdomo na wosia huo na inatakiwa kuwa ma mashahidi unatakiwa kubaki kuwa siri ili kuepusha mgogoro kwa warithi walioandikiwa.

Alisema wosia huo lazima uthibitishwe na mwanasheria ili kumsaidia mhusika kuzingatia masharti ya kukamilisha mkataba hu ambao mhusika anaweza kuomba uhifadhiwe ofis za RITA kwa usalama na ikitokea mabadiliko ya mashahidi anaweza kubadilisha.

Changula alisema wosia unaanza kufanyakazi pale mhusika anapofariki na mashahidi watawasiliana na ofisi kuwajulisha ili maandishi hayo yafikishwe kwenye kikao cha familia.

Aliongeza kuwa waosia wa tamko (mdomo) lazima ushuhudiwe na watu wanne kati ya hao wawili watakuwa ni ndugu waka karibu na wawili wanaweza kutoka nje ya wanafamilia.

Aidha alisema wanaojitoa kwenye waosia ni kundi watakaofanyajaribio la kutaka kumuua mzazi na wale ambao hawatamhudumia mzazi alipokuwa mgonjwa.

Kuhusu taratibu za usimamizi wa mirathi wanafamilia wanatakiwa kukaa kikao cha watu wasiopungua nane kati ya hao lazima wanne wawe na kitambulisho cha taifa.

Kiongozi wa kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia kwa halmashauri ya wilaya ya Itigi ,Malongo Jackson alisema lengo la kampeni hiyo ni kutoa elimu ya msaada wa kisheria pamoja na kutatua kero za wananchi.
Jackson alisema kampeni hiyo Kimkoa ilizinduliwa januari 10 mwaka huu na wamegawanyika kila wilaya kuwasikiliza wananchi kero za wananchi kupitia mikutano ya hadhara na mtu moja moja.

Alisema matatizo mengi ya wananchi wanayokutana nayo kwenye kampeni hiyo ni migogoro ya ardhi,ndoa na unyanyasaji wa kijinsia pia kampeni hiyo inawataalamu wa kisheria kutoka taaisisi mbalimbali na maofisa ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii na maofisa kutoka madawati ya kijinsi la jeshi la Polisi.

# Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria Wakumbushwa Kufanya Kazi kwa Weledi



Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Bi. Fatuma Ramadhan Mganga akihutubia wakati alipofungua Mafunzo ya Siku moja ya namna ya kutekeleza MSLAC mkoani humo, 09/01/2024.

**Na William Mabusi**
- WKS Singida

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Bi. Fatuma Ramadhan Mganga ametoa wito kwa Wataalam watakaoshiriki Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ijulikanayo kama Mama Samia Legal Aid Campaign mkoani humo wanaitekeleza kwa kutoa maamuzi na ushauri sahihi kwa wananchi watakao wahudumia ili kuwawezesha kupata haki zao.

Bi. Fatuma ametoa wito huo wakati akifungua Mafunzo ya Siku moja ya namna ya kutekeleza MSLAC mkoani humo yaliyowashirikisha watumishi wa kada mbalimbali wakiwemo Wanasheria, Maafisa ardhi, Maafisa maendeleo ya jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii kutoka Halmashauri zote saba za mkoa wa Singida na Taasisi zinazotoa msaada wa kisheria, tarehe 09 Januari, 2024 ofisi za Mkuu wa Mkoa.

"Mnaenda kutoa elimu na kutatua changamoto za wananchi zinazohusu masuala ya sheria, wasikilizeni kwa makini, wachukulieni kama wateja, wajengeeni imani na kuwapa muda wakujieleza ili wafunguke kueleza changamoto zao, ni kwa kuwaelewa ndiko kutakakowasaidia kutoa maamuzi sahihi."

Akibainisha upekee wa Kampeni hiyo Bi. Fatuma amesema "Kampeni hii ni ya kipekee sana kwani inaenda kumpa haki baba ambaye kwa muda mrefu amenyang'anywa haki yake na familia yake kuishi kwa mateso, inaenda kumpa haki mama ambaye kwa muda mrefu alikosa haki yake ya mirathi." Huku akikumbusha pia watoto wasiachwe kusikilizwa kwani yamkini kampeni ikabaini watoto ambao wamekuwa wakinyimwa haki ya shule, kuishi katika ukatili ama kubakwa.

Aidha, ameomba ushiriki wa kutosha kwa Vyombo vya Habari ili kufikisha ujumbe kwenye maeneo ambayo hayatafikiwa na Kampeni, kupitia Vyombo vya Habari Wananchi katika maeneo hayo wataweza kufikisha malalamiko yao kwa njia ya simu au kupitia njia nyingine rasmi na malalamiko hayo yakafanyiwa kazi.

Awali akitoa maelezo kuhusu utekelezaji wa MSLAC, Kaimu Mkurugenzi wa Kitengo cha Msaada wa Kisheria na Msajili wa Watoa huduma za msaada wa kisheria, Bi. Ester Msambazi amesema Singida ni mkoa wa Sita tangu kuanza kutekelezwa kwa kampeni hiyo na lengo la kutekeleza MSLAC ni pamoja na kuziba ombwe lililopo la wananchi kutotambua sheria na wapi waende wanapokuwa na changamoto za kisheria.

Utekelezaji wa kampeni hiyo unaohusisha kutoa elimu ya masuala ya sheria, msaada wa kisheria na kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa Wananchi wote na hasa wasio na uwezo wa kumudu gharama za Mawakili utazinduliwa Rasmi mkoani humo tarehe 10 Januari, 2024 na Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana, na itatekelezwa kwa siku kumi.

Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ilizinduliwa Rasmi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 27 April 2023 Jijini Dodoma na hadi sasa imeshatekelezwa katika mikoa mitano ambayo ni Dodoma, Manyara, Shinyanga Ruvuma na Simiyu na huu unakuwa ni mkoa wa Sita.



Kaimu Mkurugenzi wa Kitengo cha Msaada wa Kisheria Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Ester Msambazi akitoa maelezo kuhusu utekelezaji wa MSLAC, tarehe 09/01/2024, Singida.



Sehemu ya Washiriki wa Mafunzo ya Siku moja ya namna ya kutekeleza MSLAC wakimsikiliza Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Bi. Fatuma Ramadhan Mganga, tarehe 09/01/2024, Singida.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Bi. Fatuma Ramadhan Mganga kwenye picha ya pamoja na baadhi ya Washiriki wa Mafunzo ya Siku moja ya namna ya kutekeleza MSLAC, tarehe 09/01/2024, Singida.

# Wananchi Mkoani Singida Waendelea Kunufaika na MSLAC



Kaimu Mkurugenzi wa Kitengo cha Msaada wa Kisheria Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Ester Msambazi akitoa huduma ya msaada wa kisheria kwa Bw. Kimweri Stambuli kwenye Viwanja vya Stendi ya zamani, 11/01/2024, Singida.

**Na William Mabusi**
– WKS Singida

Kampeni ya utoaji wa elimu ya sheria na huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia Legal Aid Campaign (MSLAC) imeendelea kutoa nafuu kubwa kwa wananchi wa mkoa wa Singida katika kukabiliana na changamoto mbalimbali hususan za kisheria.

Bw. Kimweri Stambuli wa kijiji cha Iguguno ametembelea banda la Wizara ya Katiba na Sheria lililopo Stendi ya zamani kupata huduma ya msaada wa kisheria na kupatiwa ufumbuzi wa shauri lake lililodumu kwa miaka tisa sasa.

“Msaada huu ni utatuzi wa kero zinazomkabili mwananchi wa kawaida katika nchi hii, shauri langu lilikuwa na mizengwe ya kusikilizwa kwa sababu sikuwa na Wakili, lakini kupitia kampeni hii nimepata Wakili.” amesema Bw. Stambuli huku akisisitiza kampeni hiyo ifanyike nchi nzima kutatua malalamiko ya wananchi ambayo wengine wanashindwa wayapeleke wapi kutokana na kuwa mbali na vyombo vya kutolea haki.”

Katika hatua nyingine wakazi wa Kata ya Mpambala Halmashauri ya Mkalama wameshukuru kampeni hiyo kwa kuwapa uelewa kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria hususan umiliki wa ardhi kisheria kwani wamekuwa wakipokonywa mashamba yao na wananchi wachache wajanja ambao wamekuwa wakitumia mwanya huo kujinufaisha kwa kuwapora maeneo yao.

Mratibu wa utekelezaji wa MSLAC kwenye Halmashauri ya Mkalama Bw. Antony Elias amesema baada ya kukamilika kwa Kampeni hiyo timu yake itatoa majumuisho kwenye vyombo husika kuhusu maeneo yote ambayo wananchi wamelalamikia ili hatua stahiki zichukuliwe ili anayestahili haki apate haki yake bila kujali unyonge wake au kutokujua sheria.

Mtendaji Kata ya Mpambala Bw. Shadrack Makala, amekili kuwepo kwa matukio ya wananchi kupokonywa mashamba yao na kuwataka watoe ushahidi watakapoombwa kufanya hivyo ili wanaoshiriki vitendo vya uvunjifu wa sheria wachukuliwe hatua.

Naye Bw. Martine Mbasha mkazi wa kijiji cha Ipande kata ya Ipande akiwa kwenye mkutano wa utekelezaji wa MSLAC katika Halmashauri ya Itigi amesema Kampeni ya huduma ya kisheria ya Mama Samia imekuwa msaada mkubwa sana “tumefurahia elimu ya uandishi wa wosia na hasa utunzaji wake, hatukujua wosia unaweza kutunzwa na vyombo vingine kisheria lakini sasa tumeelewa wosia unatunzwa RITA tofauti na hapo wosia unaweza kuchanwa au kubadilishwa.”

Utekelezaji wa Mama Samia Legal Aid Campaign (MSLAC) umezinduliwa mkoani humo na Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana tarehe 10 Januari, 2024 na itatekelezwa kwa siku kumi katika Halmashauri zote saba.



Wananchi waliotembelea banda la Wizara ya Katiba na Sheria kwenye viwanja vya Stendi ya zamani wakipatiwa huduma ya msaada wa kisheria, tarehe 11/01/2024, Singida.



Mratibu wa MSLAC Halmashauri ya Mkalama Bw. Antony Elias akitoa elimu ya sheria kwa wananchi wa Kata ya Mpambala, 12/01/2024.



Bw. Martine Mbasha mkazi wa kijiji cha Ipande kata ya Ipande Halmashauri ya Itigi akitoa shukrani zake kwenye mkutano wa utekelezaji wa MSLAC baada ya kupata elimu ya uandishi na utunzaji wa Wosia, 13/01/2024.

# Wananchi Washauriwa Kuibua Kero Nzito Nzito Kuitwisha MSLAC



Afisa Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida Bi. Paskazia Kyaruzi akitoa mada kuhusu masuala ya ardhi, 16 Januari, 2024 Kijiji cha Ikhanoda.

**Na William Mabusi**
- WKS Singida.

MIGOGORO ya ardhi imetajwa kuwa ni ndio moja ya kero kubwa kwa wananchi wilayani Iramba Mkoani hapa na imesababisha kutumia muda mwingi kutafuta haki hiyo maeneo mbalimbali ya utoaji haki.

Hayo yalibainishwa wakati wa mkutano wa hadhara kati ya wananchi na timu ya kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia uliofanyika Kata ya Shelui Wilaya ya Irimba Mkoani Singida.

Kero hiyo ya migogoro ya ardhi imetajwa kuwa ni kubwa kwa wananchi hao na imesaababisha kutumia muda mwingi kuitafuta haki hiyo kwenye maeneo ya utoaji haki. Mmoja wa wananchi wa Kata hiyo Johashi Shimikila akizungumza kwenye mkutano huo alisema kero hiyo inaongoza kati ya kero nyingi walizonazo wananchi wa wilaya hiyo.

Shimikila alisema wanashuru wajumbe wa kampeni hiyo kufika hapo na kilio chao



Wakili wa Serikali Caren Rwebangila kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoa wa Singida akitoa mada ya ndoa kwa wakazi wa Vijiji vya Ikhanoda na Msimihi Kata ya Ikhanoda, 16 Januari, 2024.



Afande Veronica Masele kutoka Dawati la Jinsia na Watoto Halmashauri ya Wilaya ya Singida akitoa mada ya ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Ikhanoda, 16 Januari, 2024.

namba moja ni kero ya ardhi ambayo imesabaisha kupoteza mud na fedha kiitafuta. Kadhalika alisema wanamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kujna na kampeni hiyo ambayo inatoa fursa kwa wananchi kusikilizwa na kusaidiwa kupata haki zao.

*“Binafsi nimetoa kero yangu hii ambayo imekuwa ikinisumbua mimi na wananchi wenzangu ya migogoro ya ardhi hivyo kupitia kampeni hii nimepata Imani ya kuhudumiwa”.*
alisema.

Aliitaja aina ya migogori iliyopo kuwa ni kugombea mipaka ya mashamba na wengine kudhulimiwa ardhi kutokana na kushindwa kuwalipa mawakili wa kuwasaqidia kesi zao.

Aliongeza migogoro mingine ni kucheleweshwa kwa hati za maeneo yao waliopimiwa jambo ambalo linawachelewesha kuendeleza maeneo yao .

Mkazi mwingine Sada Salula alisema wanawake wengi waliofiwa na waume wao hasa maeneo ya Vijijini wamekuwa wakinyang’anywa ardhi kwa madai kuwa hawana haki ya kumiliki.

Sada alisema wajane hao wamekuwa wakifukuzwa kwenye familia waliyokuwa wakiishai na wenzao wa kwa madai kuwa mila haziruhusu mjane kumiliki ardhi.

“Mimi hapa ni miongoni mwa wajane niliyenyang’anywa ardhi baada ya mume wangu kufa kwa sa nahangaika na watoto wangu nimeshafukuzwa nimeona nifike hapa kutoa kilio change kwenye kampeni hii ya Mama Samia”aliangua kilio.
Mkuu wa Wilaya ya Iramba ,Suleiman Mwenda alikiri kuwepo kwa malalamiko hayo ya ardhi na kuwataka wananchi kufika kwenye kampeni hiyo ili kupata haki yao.

“Kwa kweli katika malalamiko mengi yanayokuja ofisini kwangu kama Mkuu wa Wilaya ni masuala ya ardhi,ardhi imekuwa tatizo sana katika wilaya yetu ya Iramba ,kesi ni nyingi mno kutokana na uhaba wa watoa huduma za kisheria kumeibuka na wanasheria feki wanaowatapeli wananchi”alisema

Mwenda alisema anaamini kupitia kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria mama Samia itawasaidia wananchi wengi kupata haki zao kwa sababu inawataalamu wa kila idara na aliwataka wananchi ahao kujitokeza mbele ya timu hiyo ili kusikiliza na kutatuliwa kero zao zinazowakabili.

Kiongozi wa kampeni ya huduma ya msaadw wa kisheria ya mama Samia Wilaya ya Iramba ,Godfrey Ngangaji alisema kampeni hiyo ilizinduliwa Aprili 2023 na inaendelea kuzinduliwa kila Mkoa mpaka sasa imefika Mikoa sita.

Ngangaji alisema lengo la kampeni hiyo ni kuwasaidia wananchi kupata haki zao na imekuwa ikifanyakazi na watu wa idara zinazotoa haki ambazo ni mahakama,wanasheria,jeshila Polisi,Maofisa maendeleo ya jamii,Ustawi wa jamii ,Ofisi ya Mwendesha mashtaka na watalamu wengine wa sheria.

# Tutaendelea kutoa Elimu na Kutatua Changamoto za Kisheria kwa Wananchi

**Na William Mabusi**
– WKS Singida



Bi. Basuta Milanzi akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa MSLAC katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida kwa Katibu Tawala wa Wilaya Singida Bi. Naima Bakari Chondo, tarehe 19 Januari, 2024

Katibu Tawala wa Wilaya Singida Bi. Naima Bakari Chondo ameahidi kutekeleza changamoto za wananchi ambazo hazikutatuliwa katika kipindi cha kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ili kuendelea kutatua migogoro kwenye jamii.

Bi. Naima ametoa kauli hiyo baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa Kampeni hiyo iliyokuwa inafanyika kwenye Halmashauri yake kwaniaba ya Mkuu wa Wilaya ya Singida, tarehe 19 Januari, 2024.



Katibu Tawala wa Wilaya Singida Bi. Naima Bakari Chondo, akipokea taarifa ya utekelezaji wa MSLAC katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida, tarehe 19 Januari, 2024

Aidha, akiongelea changamoto za kesi za ukatili wa kijinsia amesema, "ipo changamoto ya kesi za ukatili wa kijinsia na kuzifanya kuwa ngumu kuendesha na wakati mwingine kutofika mwisho kutokana na Mahakama kukosa ushahidi wakati ni kweli kabisa kitendo cha ukatili kimefanyika, niwaombe waathirika na wazazi kutokukubali kumaliza kesi kifamilia, maamuzi ya namna hii hayamtendei haki mwathirika."

Katika hatua nyingine Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Singida Bi. Esther Chaula amesema kwa kutumia rasilmali kidogo waliyonayo wataendelea na utoaji elimu ya sheria kwa wananchi.

"Maeneo yaliyobaki tutajipanga na watu wangu kwa kadri tutakavyoweza kutumia rasilmali tuliyonayo na kupitia mikutano kutoa elimu ya kisheria na kuendelea kutatua migogoro kwenye jamii. Unakuta mwananchi hakuridhika na uamuzi wa Mahakama, kwa kutokujua masuala ya sheria anarudi tena Halmashauri. Wakati mwingine mwananchi anafanyiwa ukatili bila kujua ni ukatili na wakati mwingine hata akijua ametendewa ukatili hajui afanye nini." Alisema Bi. Chaula.

Ameshukuru Wizara ya Katiba na Sheria akisema kitendo cha kuwafuata wananchi kuwapa elimu na huduma ya msaada wa kisheria kinawadhihirishia kwamba Serikali iko karibu na wananchi. "Kupitia hii kampeni mmetuongezea maarifa kwani watumishi mliokuwa mnazunguka nao kutekeleza kampeni kuna jambo wamejifunza, hivyo tutawatumia kufika maeneo ambayo hamkuweza kufika."

Kampeni ya Kitaifa ya kutoa elimu na huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia Legal Aid Campaign ilizinduliwa Mkoani Singida na Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana tarehe 10 Januari, 2024 na kufanyika kwa siku kumi kwenye Halmashauri zote saba za mkoa huo na leo ndiyo imehitimishwa.



Bw. Athuman Msosole akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa MSLAC katika Manispaa ya Singida kwa Katibu Tawala wa Wilaya Singida Bi. Naima Bakari Chondo, tarehe 19 Januari, 2024



Katibu Tawala wa Wilaya Singida Bi. Naima Bakari Chondo, akiongea baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa MSLAC katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida, tarehe 19 Januari, 2024



Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Singida Bi. Esther Chaula akimsikiliza Bi. Basuta Milanzi wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa MSLAC katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida, tarehe 19 Januari, 2024.

# Matukio Katika Picha



Mwanasheria Mkoa wa Singida Bi. Nasemba Mkambazi akitoa huduma ya msaada wa kisheria kwa Bi. Juliana Tomasi kwenye Viwanja vya Stendi Mpya, Singida tarehe 16 Januari, 2024.



Afisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Singida Bi. Judith Misango akitoa huduma ya msaada wa Kisheria Kata ya Mungumaji, 15 Januari, 2024.



Afisa Usajili RITA Bw. Juma Abdallah akitoa elimu kuhusu cheti cha kuzaliwa na cheti cha kifo kwa wanafunzi wa shule ya Msingi Mungumaji katika Kata ya Mungumaji, 15 Januari, 2024.



Wakili wa Serikali kutoka Tume ya Kurekebisha Sheria Bi. Jacqueline Nungu akitoa huduma ya msaada wa kisheria kwenye Viwanja vya Stendi Mpya, Singida 15 Januari, 2024.



Wakili wa Serikali Bw. Athuman Msosole akitoa huduma ya msaada wa kisheria kwenye Viwanja vya Stendi Mpya, Singida 15 Januari, 2024.






Wanachi waliofika banda la Wizara kwenye Viwanja vya Stendi ya zamani wakipatiwa huduma ya msaada wa kisheri, 15 Januari, 2024.



Waziri wa Katiba na Sheria Dk Pindi Chana (kushoto) akimsikiliza Mtendaji  Mtendaji Mkuu wa Mahakama Tanzania Prof Elisante Ole Gabriel wakati alipotembelea banda la ofisi hiyo kwenye mwendelezo wa  uzinduzi wa  Kampeni ya huduma ya masada wa kisheria ya Mama Samia ilizunduliwa Mkoa wa Singida jana ,uzinduzi huy ulifanyika Manispaa ya Singida .



Waziri wa Katiba na Sheria Dk Pindi Chana (kulia) akisalimiana na viongozi wa dini Mkoa wa Singida kutoka kushoto Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dk Syprian Hilinti na Shehe wa Mkoa wa Singida Issah Nassoro walipokutana kwenye uzinduzi wa Kampeni ya huduma ya masada wa kisheria ya Mama Samia iliyozunduliwa jana Manispaa ya Singida.



Waziri wa Katiba na Sheria Dk Pindi Chana (kulia) akiwapungia mono wafanyakazi wa wizara hiyo walipokutana kwenye uzinduzi wa  Kampeni ya huduma ya masada wa kisheria ya Mama Samia ilizunduliwa Mkoa wa Singida jana ,uzinduzi huy ulifanyika Manispaa ya Singida .

